

Kukataa Meza Ya Bwana (Neglect Of The Lord's Supper)

Na

John Kombo

Kukataa Meza Ya Bwana (Neglect Of The Lord's Supper)

Na

John Kombo

December 6, 2013

Kukataa Meza Ya Bwana (Neglect Of The Lord's Supper)

Meza ya Bwana ni tendo la ibada lililobarikiwa. Hii ni:

- Muda wa “kuelekeza” kwamba tunataka kula, “kwa ukumbusho” wa Bwana wetu (1 Kor. 11:23-25).
- Ni wakati wa “kushukuru” kwamba tunachukua muda tukimfikiria mtu ambaye mwili wake na damu vilimwagika msalabani “*kwa ajili yetu*” (1 Kor. 11:23-25).
- Ni wakati wa “kutangaza” kwamba “*tunakumbuka*” mauti ya Bwana tunapokula (1 Kor. 11:26).
- Ni wakati wa “kujichunguza” tunapaswa kujichunguza wenyewe na kushiriki meza ya Bwana inavyostahili (1 Kor. 11:27-32).
- Na mwisho, wakati wa “kushirikiana” kwamba tunapaswa kuwajali wengine katika huku kula (1 Kor. 11:33-34).

Kwa sababu ya ukweli huo hapo juu, hatupaswi kuacha meza ya Bwana, lakini mhimu sana, tuifanye kuwa wakati muhimu ya jumaa. Meza ya Bwana inatukumbusha mambo makuu mawili: “upendo” wa Mungu na “Sheria” ya Mungu.

“Upendo” wa Mungu

Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwaa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu tulipokuwa tungali wenye dhambi (Rum. 5:8; Yoh. 3:16; 1 Yoh. 4:7-11). Meza ya Bwana imetengenezwa kutusaidia kutazama kwa kina, ndiyo, alama ya upendo. Shukrani, kila mmoja wetu anaweza kusema kama Paulo “*Kristo alitupenda na akajitoa kwa ajili yangu*” (Gal. 2:20) Yesu alitufanyia yafuatayo:

- Alijitoa mwenyewe kwa ajili ya dhambi zetu ili aweze kutukomboa (Gal. 1:4).
- Alijitoa mwenyewe dhabihu kwa ajili yetu (1 Tim. 2:6).
- Alijitoa mwenyewe kwamba aweze kutuokoa (Tito 2:14).

Sheria ya Mungu

Tunapokula meza ya Bwana ipasavyo tunaonyesha katika “damu” ya Yesu. Alitwaa kikombe akasema. “*kikombe hiki ni agano jipya*”

imwagikayo kwa ajili yenu” (Luka 22:20). Angalia ukweli kwamba alitwaa kikombe na Biblia inasema **alitwaa kikombe** na kusema **“kikombe hiki”**; hakutwaa vikombe na kusema vikombe hivi. Tena, “Damu yake “ilimwagika” kwa ajili yetu.

Kuna mateso mengi ambayo Bwana wetu aliyapitia; mgongo wake ulikuwa na alama za viboko (Mat. 22:26) na Isa. 53:5); mbavu zake ziliachwa wazi kwa mkuki wa askari wa Rumi.

Yote hayo hapo juu yalimtokea Yesu Kristo kwa sababu alijitoa dhabihu kwa ajili ya:

- “Ondoleo” la dhambi zetu (Mat. 26:8).
- “Kututhibitisha” (Rum. 5:9).
- “Wokovu wetu” (Rum. 5:9).
- “Ukombozi wetu (Efe. 1:7).
- “Upatanisho” (Efe. 2:13).
- “Utakaso wetu” (Ebr. 10:39)
- “Usafi wetu” (1 Yoh. 1:7).

Hatupaswi kusahau kujumuisha kwamba “taasisi” kuu katika dunia – kanisa la Bwana – lilinunuliwa (Mdo. 20:28). Tunaposhiriki Meza ya Bwana ipasavyo tunaonyesha kifungo tunachoshiriki pamoja na Yesu Kristo. Meza hii inaelezwa kama komunio pamoja na damu na mwili wa Yesu Kristo (1 Kor. 10:16). Inatuunganisha katika moyo na mawazo tunaposhiriki. Huu ni wakati wa kipekee ya “ushirika” pamoja na kila mtu, na Kristo. Alipoanzisha Meza, Yesu alisema, *“sitakunywa tangu sasa uzao huu wa mzabibu hadi siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba”* (Mat. 26:29). Ni ajabu sana na inahamasisha kujua kwamba Bwana wetu yuko pamoja nasi tunaposhiriki katika kila tendo lo lote la ibada. Tuungane na Paulo katika maneno yake na kufikiria katika meza ya Bwana kama wakati tunapojingiza katika “Ushirika wa mateso ya Yesu” (Fil. 3:10). Mungu atubariki sote tunapojifunza somo hili, ili **TUSIJE TUKAACHA MEZA YA BWANA.**

John Kombo Nandwa

Kanisa la Kristo

Barut, Nakuru, Kenya

